

Je, Nitaulizwa Nini Nitakapopigiwa Simu ya Kufuatilia Mtagusano?

Tunataka ujihisi salama unapojibu simu ya kufuatilia mtagusano na kujua maswali ya kutarajiwa. Ikiwa umekaribiana na mtu aliye na COVID-19, mfuatiliaji wa mtagusano atakufikia kwa njia ya simu. Watakwambia wametoka katika mamlaka ya afya ya eneo au umma ya kabila lako. Simu hiyo haitakuwa imerekodiwa kiautomatiki. Utazungumza na mtu halisi.

Mfuatiliaji wa mtagusano atakuuliza:

- ✓ Ikiwa unahitaji mkalimani kwa lugha nyengine isiyo Kiingereza
- ✓ Jina lako, tarehe ya kuzaliwa na unakoishi
- ✓ Ikiwa unazo dalili zozote za COVID-19
- ✓ Ikiwa unahitaji mahali pa kukaa
- ✓ Ikiwa unahitaji chakula au unayo mahitaji mengine ya kukusaidia kukaa nyumbani
- ✓ Ikiwa wanaweza kuwasiliana nawe kila siku ili kufuatilia dalili na mahitaji yako
- ✓ Kuhusu tabaka la rangi yako, kabila, lugha na taarifa kuhusu ulemavu.



Mfuatiliaji wa mtagusano hatawahi kukuuliza kuhusu:

- ✗ Nambari ya Usalama wa Kijamii
- ✗ Akaunti ya benki au nambari ya kadi ya manunuzi
- ✗ Hali ya uhamiaji.

Anayepiga simu hata:

- ✗ Sema unahitajika kulipia huduma hii au
- ✗ Kutoa vitisho vya kukuweka wewe au familia yako gerezani ikiwa hauzungumzi na mfuatiliaji wa mtagusano.

Ikiwa unashuku ulaghai, kata simu.

Usijibu simu zingine zinazopigwa kutoka kwa nambari hiyo.

Ripoti tukio hilo na ujifunze vidokezo vya kuzuia ulaghai kwa kutembelea Tume ya Shirikisho la Kibiashara mtandaoni kwa www.consumer.ftc.gov.

Unaweza pia kujifunza kuhusu mchipuko wa utapeli na kuripoti tukio hilo kwa Idara ya Haki ya Oregon mtandaoni kwa www.OregonConsumer.gov.



Oregon, hebu tujibu simu.

Kwa watu walio na ulemavu au watu wanaozungumza lugha nyingine isiyo Kiingereza, OHA inaweza kutoa hati katika mifumo badala kama vile lugha zingine, maandishi makubwa, breli au mfumo unaopenda. Wasiliana na Mavel Morales kwa 1-844-882-7889, 711 TTY au OHA.ADAModifications@dhsosha.state.or.us.

OHA 2359D Swahili (06/10/2020)

Oregon
Health
Authority